


MMOJA WA WATU

KATILI SANA MJINI

 Ndugu Carlson, na wageni waheshimiwa, Ndugu David duPlessis, na Ndugu Roy Weed, Ndugu Mattsson-Boze, na wote, tuna furaha kuwa hapa asubuhi ya leo ili, katika utumishi wa Bwana.

² Nami ninajisikia tu nimeshiba asubuhi ya leo kusikia shuhuda hizi zote nzuri sana, kuona jinsi zinavyowafanyia watu. Nilikuwa nikisikia ushuhuda wa mlevi sugu na kumtazama Rosella ameketi pale, nione ulikuwa na matokeo gani kwake; nikimwangualia ndugu huyu Mbaptisti hapa, unabii wake ambao Mungu alimpa ya kwamba kulikuwa kunakuja mfagilio kote nchini, nikaona ulivyowafanyia watu, kumsikia Roho Mtakatifu akinena kwa lugha na kufasiri, na kutuambia tuko mwisho kabisa, uko papa hapa sasa, na jinsi ambavyo Mungu alimpa ujumbe huo, kisha akamwingiza moja kwa moja ndani yake.

³ Mnaona, jinsi tu ambavyo kama tungeangalia tu kote na kuona jinsi Mungu anavyotenda kazi kitukufu, na kufanya yale hasa aliyosema angefanya, jinsi ambavyo hatuna budi kuamka, na kukumbuka, si katika siku za usoni, ni sasa, tuendelea tu kusonga mbele, sasa hivi, tu—tuendelea tu kusonga mbele.

⁴ Basi msikieni Ndugu David pale, nina hakika mtasikia mambo makuu alasiri ya leo kwenye mkutano wa alasiri, wakati Ndugu duPlessis. . . ambaye nilikuwa nikizungumza habari zake hivi majuzi usiku jukwaani, halafu basi jana usiku huyo hapo, papo hapo, sikuwa na fununu kwamba angekuja, lakini daima umekuwa ni ushirika mzuri sana wangu na Ndugu David, katika safari hii ya ulimwengu na huduma katika siku hii ya mwisho.

⁵ Nalo tawi la Chicago, hapa, limekuwa zuri sana kwangu, na mara nyingi nimekuwa hapa katika ushirika huu, ninauthamini kila wakati. Kila wakati ninapozungumza kuhusu kwenda Chicago, mbona, Billy na Leo, na hao wote huruka tu kwa furaha, wananinii tu, wanapenda kufika Chicago. Walisema tu, “Tunajisikia vizuri sana huko Chicago, kwa namna fulani.” Kwa hiyo, tuna furaha sana.

⁶ Nilikuwa nikiwazia hapa dakika chache zilizopita juu ya rafiki yangu halisi, wa kifalme, Ndugu Roy Weed. Ninamkumbuka akisimama karibu nami katika majira ya haja wakati nilipoingia hudumani kwa mara ya kwanza, na jinsi alivyosimama pamoja nami wakati haikumlazimu kufanya hivyo, lakini, Mungu tu, kutokana na wema wa moyo wake alisimama moja kwa moja pamoja nami.

7 Na kila wakati ninapowazia juu ya Assemblies of God, ama—ama kukutana na ndugu fulani, labda, kwamba nawazia alifanya jambo ambalo kamwe halikuwa lile alilipaswa kufanya, nami nadhani anawazia vivyo hivyo kunihusu mimi, lakini daima mimi huwazia juu ya Roy Weed. Mnaona, nafikiri hapo kwamba sisi. . . Akaweka bega lake mahali fulani na kusimama pamoja nami majira ya ninii, wakati mimi, ilibidi uamuzi ufanywe, kwa sababu nilikuwa nimefanya uamuzi juu ya neno langu lililoahidiwa, Ndugu Roy aliwazia labda mbele ya ndugu zake huenda ikasababisha shutuma ama kitu fulani, ndipo Ndugu Roy akasimama moja kwa moja pamoja nami jukwaani; kamwe sitamsahau.

8 Ndipo ninafikiri sasa kwamba mimi, uh, Bwana amenisaidia kuwa na marafiki, kila kitu, huenda nikamwona rafiki mwingine ambaye ningeweza kumsaidia namna hiyo pia, nikikumbuka nilikotoka pia. Nafikiri sote tunapaswa kufanya hivyo, kukumbuka mahali tulipochongewa.

9 Sasa, hatuna wakati wa kutosha hapa kwangu kuhubiri, tunajua hilo, maana mimi huchukua muda mrefu sana. Nami nilikuwa tu nikiwazia, laiti baadhi ya ndugu wangekaa huko juu, mwajua, ili kwamba nilipofika kule juu, ningeweza kutoa tu ushuhuda na—na kuketi chini. Lakini sasa, inaniachia wakati wa kusoma Maandiko, nafikiri, kutoka nje. Sitaninii. . . hatutaki kukaa zaidi ya saa tano, kama tunaweza kusaidia, kwa sababu nafikiri huo ndio wakati; Ndugu Carlson ni mwema sana.

10 Billy ameketi hapa akisafisha koo hili na kunicheka, kwa sababu yeye bado hafikirii ninaweza kuhubiri mahubiri ya dakika thelathini, niondoke jukwaani. Lakini, sikuzote hunicheka, kwa sababu alisema, “Baba, najua,” kasema, “sasa, nilikutana nawe huko nje usiku wa leo, ulisema dakika thelathini, lakini niliangalia zile dakika thelathini,” kasema, “hukuwa umeanza wakati dakika thelathini zilipotimia.”

11 Kwa njia ya kusoma Maandiko, kusudi tuweze kuingia moja kwa moja ndani yake. . . Na makaribisho hayo mazuri sana ambayo ninyi watu mlinipa, kamwe sitasahau hayo, sitasahau, kamwe sitasahau. Nami ni—ningewafanyia lolote.

12 Wakati mwingine mimi. . . Sasa, hili kwa namna fulani ni juu yetu watu wa nyumbani hapa, kama tunavyolisema huko kusini. Wakati mwingine mnanisikia nikikata, na kwa kweli, mimi huenda nyumbani na kuketi chini, na wakati mwingine kuchukua moja ya kanda hizo, na kusema, “Hakika, sikusema hivyo. Hakika, nisingeweza kusema hivyo.” Na—na halafu ninawazia, “Vema, yale niliyosema, nimesema. Na ilikuwa—ilikuwa chini ya uvuvio, kadiri nijuavyo mimi, uvuvio, kwa hiyo kamwe siionei haya.” Wala si—simaanishi kamwe kumwudhi mtu yeyote, kama hiyo ingekuwa ndiyo nia ya—yangu, basi

lengo langu si sahihi, mnaona. Mi—mimi tu . . . si—singekuwa . . . kufanya hivyo.

¹³ Lakini wakati mwingine mimi hupanda pale, ninawazia, “Nitasoma somo . . .” Nina yapata mafungu matano hapa niliyotaka kuyazungumzia asubuhi ya leo, mnaona, nami ni—nikasema, “Vema sasa, kama nina dakika thelathini, nitazungumza juu ya *hili*; kama nina dakika ishirini, nitazungumzia *hili*; nina saa moja na nusu, nitazungumzia *hili*.”

¹⁴ Na kwa hiyo nilipata somo langu la dakika thelathini hapa asubuhi ya leo. Bila shaka, ninaamini katika kuzidisha, mwajua, lakini muda si mrefu vya kutosha, kwa hiyo, lakini hebu tufungue, kama mngetaka, katika Kitabu cha Luka Mtakatifu, mlango wa 7 na kifungu cha 40:

*Yesu akajibu akamwambia, Simoni, nina neno
nitakalo kukwambia. Akasema, Mwalimu, nena.*

¹⁵ Tukijua ya kwamba mfumo wa Mawasiliano ni mbaya sana, basi nadhani mnaweza kunisikia vema huko nyuma sasa? Ndugu yetu hapa, aliyeketi hapa, alikuwa na wasiwasi usoni, kwa sababu ninii yake . . . milimwangelia na kumhurumia, kisha nikaangalia jinsi wimbo huo ulivyomchangamsha muda mfupi uliopita, dada huyo alikuwa akiimba, na jinsi ambavyo kuna neema, tunaamini hilo, neema ya ajabu ya Kristo.

¹⁶ Nami nilifikiri labda asubuhi ya leo tungezungumza juu ya somo ambalo lingekuwa, labda, kwa kifupi tu, kidogo ni mchezo mdogo wa kuigiza, kitu kama hicho, juu ya *Mmoja wa Watu Katili Sana Mjini*. Sasa, hilo ni somo kweli la kuchukua kwenye kiamshakinywa cha wafanyabiashara. Lakini labda baadhi ya watu hawajui kabisa mtu katili ni nini, kwa hiyo tu—tungetaka kuzungumza juu ya mmoja.

¹⁷ Hapana shaka jua lilikuwa likitua wakati yule tarishi alipowasili. Ilikuwa ni siku kuu, naye Yesu alikuwa akiwaombea wagonjwa, akihubiri, na, loo, watu walikusanyika ili tu kushikilia Neno moja ambalo Yeye alisema. Ningalipenda kuwako huko. Mara nyingi nimeshangaa jinsi ingelikuwa nilipomsikia akinyosha mikono yake, na kusema, “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo.” Labda hata sitaishi kuona siku watakapounasa mtetemo huo kusikia jinsi unavyosikika, halafu bila kujua Kiebrania, nisingeweza kuufahamu. Lakini ninatumaini Siku hiyo nitamsikia akisema, “Ulifanya vema, mtumishi Wangu mwema na mwaminifu.”

¹⁸ Nao umati ulikuwa hautulii, na wengi hawakuwa wameombewa, nao walikuwa wakishangaa angekuwa wapi kesho yake, kwa sababu hawakujua siku moja kwa nyingine mahali Yeye angekuwa, Roho angempeleka.

19 Nao wanafunzi walikuwa wamechoka mno kwa kuwasukuma watu nyuma, na kusema, “Twa—twaomba tu msisukumane, iweni tu na kicho, naye Bwana wetu atawafikia upesi tu awezavyo.”

20 Basi huyu tarishi akaja, na hapana shaka alizungumza na, hebu tuseme, Filipino, na hapana shaka alisema, “Nina u—ujumbe kwa ajili ya bwana wako. Ninatoka kwa mfanyabiashara, na sina budi kumfikishia ujumbe huu.”

21 Naye Filipino huenda alisema kitu kama hiki: “Bwana we—wetu amechoka sana, bwana, kwa sababu amekuwa na shughuli nyingi siku nzima. Tumeshuhudia kwa macho yetu miujiza mikubwa na ishara ambazo Mungu amefanya kupitia Yeye.”

22 Lakini huyo tarishi hakuvutiwa na miujiza hiyo, alivutiwa tu na yale bwana wake alikuwa amemtuma kusema. Hatimaye, Filipino, akiwa mwungwana Mkristo, akapenya akapita pamoja na huyo tarishi, mpaka akafika Mbele za Bwana, naye akasema, “Kijana huyu ana ujumbe kutoka mji mwingine, ambako kuna mtu mashuhuri ambaye. . . anataka kuzungumza Nawe juu ya bwana wake.”

Nami ninaweza kuona macho yaliyochoka, yaliyodhoofika ya Bwana wetu wakati alipogeuka na kusema, “Unataka kusema nini?”

Mara nyingi nimewazia, “Vipi kama ningekuwa tarishi huyo?”

23 Lakini akasema, “Bwana wangu amekupa heshima: Ana karamu kuu, naye anataka uwe mgeni wake maalum kwenye karamu hii. Nasi tungetaka utuahidi ya kwamba ungekutana nasi katika siku *fulani*. Ni,” labda, “shughuli ya kila mwaka, na—na kati ya watu wote, yeye alikuchagua wewe uje.”

24 Mwajua, ninaamini kama ningalikuwa nimesimama pale karibu hivyo na Bwana Yesu, ningesahau yote kuhusu yale Simoni aliyokuwa ameniambia niseme. Jambo la kwanza ningalisema, lingekuwa, “Bwana, unirehemu mimi, mwenye dhambi.”

25 Lakini hivyo ndivyo wengi wetu wanavyofanya, tunajisikia kwamba shughuli zetu za kila siku na mahitaji ya kazi yetu ni muhimu zaidi kuliko kitu kingine chochote. Nami ninaamini, kama tukiwahi kwenda Mbele za Mungu, sifa zetu za duniani, washiriki wetu wa duniani, ujumbe wetu, ama kazi yetu zinapaswa kuwa ndizo za mwisho, hebu na tutoe maungamo yetu Kwake.

26 Loo, ningalipenda kuanguka miguuni Pake pale, na kusema, “Nina ujumbe kutoka kwa bwana wangu, lakini kwanza nina ujumbe, pia: Unirehemu, Ee Mungu, mimi ni mwenye dhambi. Nami ninajua ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, nami

nimetamani nafasi hii, na sasa ninapiga magoti hapa miguuni Pako, unirehemu.”

²⁷ Lakini yeye, kama wengi wa vijana siku hizi, alikuwa na mambo mengine niani mwake. Basi alitaka kuutoa huo ujumbe, naye alikuwa amechoka, nayo miguu yake ilikuwa na jasho kwa kukimbia, na, kufika kule, kwa sababu hakujua mahali Mwalimu angekuwa kesho yake, kwa hiyo akampata mahali fulani, ambapo angeweza kuongea Naye.

²⁸ Ninawatakeni mwone m—mtazamo ambao Yesu alichukua kwa mtu huyo. Hapana shaka alimwangalia huyo kijana wa kisasa wa siku hizo kwa heshima, naye alijua kwamba labda anapaswa kuomba msamaha wa dhambi zake. Lakini na liwe liwalo, Yeye, ratiba Yake yote kuu, hakuwa na ratiba ya duniani nijuavyo mimi, bali kufanya tu mapenzi ya Mungu katika kila hatua aliyopiga, bila kujua mahali hasa ambapo Baba angemwita kesho yake, bali alipenda na alikuwa tayari kwenda, katika ratiba Yake yote yenye shughuli nyingi na yote aliyopaswa kufanya, angali alielekeza macho Yake yenye uchovu kwa tarishi huyu, kasema, “Nenda, kamwambie bwana wako nitakuwa huko.”

²⁹ Sasa, hapana shaka moyoni mwangu, nami ninaamini katika wengi wetu siku hizi, ila kwamba Yesu alijua kilichokuwa kikimngojea afikapo kule, kwa sababu alijua siri ya moyo wa wanadamu. Naye alijua ya kwamba Simoni alikuwa na hila, kwa maana mtu, Mfarisayo, angewezaje kuwa na ushirika wowote, na atake kumwona Yesu, ambaye alimchukia? Mafarisayo hawakuwa na uhusiano wowote na Yesu.

³⁰ Na unapowaona watu ambao, wa namna hiyo, ambao, watu wa ulimwengu wanaotaka kukualika nje mahali fulani kwenye karamu, kukupeleka kwenye karamu ya Krismasi, baadhi yenu Wakristo mnaomfanyia Bwana kazi, na ninii yako, inakubidi kufanya kazi hapa kwa ajili ya riziki yako ya kila siku, unapomsikia bosu wako, anayekunywa pombe, anayevuta sigara, hufanya mizaha michafu miongoni mwa watu, wakati anapokualika kwenye karamu fulani, ana njama fulani. Giza na nuru havishiriki pamoja.

³¹ Unapomwona msichana mdogo mwenye umri wa kama miaka mitano akishirikiana na nyanya yake, kuna kasoro. Unaona? Sasa, yeye ama ni kipenzi cha nyanya, ama nyanya ana maskini kifurushi cha peremende mahali fulani. Kuna tofauti kubwa sana katika umri wao, maskini msichana huyo anataka kuzungumza juu ya wanasesere, na kadhalika, naye nyanya ni mwanamke mkongwe, ana jambo lingine la kuzungumzia. Kwa hiyo mnaona, maskini huyo msichana, kama vile tungesema, ana siri mahali fulani. Kuna kitu fulani anachongojea kwa nyanya.

³² Na wakati ulimwengu unapojaribu kukupigapiga begani na kusema, “Waweza kuja *huku* tafadhali?” ama kitu fulani, kuna

kasoro mahali fulani.

³³ Naye Yesu alijua wakati Simoni huyu, Farisayo, alipomwalika kwenye dhifa ya kutwa, kulikuwa na kasoro mahali fulani, hata hivyo katika hayo yote, Yeye alikuwa tayari kwenda. Yeye ni...Sikuzote atakuja mahali anapoalikwa, bila kujali hali ya mambo na kile anachojua kitatendeka, ukimwalika, Yeye atakuwepo. Naam, unaweza kutegemea hilo.

³⁴ Sasa, yeye alisema, wakati ulipokaribia kwa ajili ya dhifa hii kuu...Ninaweza kuwazia nikimwona Farisayo huyu, ambaye alikuwa ni tajiri. Hakukuwako na tabaka la kati la watu siku hizo, kama vile labda huko India na kwingine sasa, ambako kweli ni maskini na matajiri. Wale walio matajiri ni *matajiri* kweli, na wale walio maskini, ni maskini hohehahe, hakuna watu wa tabaka la kati. Basi matajiri walikuwa na pesa zote, maskini hawakuwa nazo hata. Na wakati mwingine, wakati hawa matajiri wangeweza kufanya dhifa, *kweli* walifanya dhifa halisi.

³⁵ Kwa hiyo wakati, tarehe iliyowekwa, ilipokaribia, hapana shaka kwamba Simoni aliiweka kwenye wakati ambapo zabibu zake zote zingekuwa zimeiva, na kungekuwako na ha—harufu nzuri sana kila mahali kwenye mashamba makubwa na mizabibu yaliyojaa zabibu zilizoiva, huku nyuki wakivuma. Nao wangechinja wana-kondoo wao walionona na kula nyama choma. Nao kweli wangeweza kuleta divai nzuri sana, na kuzitandaza kwenye uwanja wa mbele, na kuwaalika wageni wao matajiri, na kweli walikuwa na wakati *mzuri* sana, ila maskini hata wasingeweza kuingia ndani ya hilo lango.

³⁶ Ndipo hiyo siku ilipowadia, nayo dhifa ikawa tayari kabisa, nao...wanyama walichinjwa, nayo majiko ya nyama choma yalikuwa yakifuka moshi kwa nyama zilizochomwa vizuri sana, viungo vizuri juu yake. Ninawazia maskini wakipita, huku wakiramba midomo yao.

³⁷ Basi kuja kwenye moja ya karamu hizi, ilibidi ualikwe, mwaliko. Halafu unapokuja, mbona, wao sikuzote, wao... ilibidi ukaribishwe unapokuja. Wakati...Mtu fulani alikuwa pale kukulaki achukue mwaliko wa—wako, nao walikuandikisha, wale waliopaswa kuwa kule, na “Huyu ni *Nanii wa nanii*,” na kutia alama jina lako, na, “amewasili.”

³⁸ Na—nami ninakumbuka, nilipokuwa nikisoma jinsi walivyowatumbuiza katika siku hizo huko Mashariki, watu, walisafari ama kwa mkokoteni, ama kwa kupanda farasi, ama—ama kwa kutembea. Matajiri wangeweza kuendesha kibandawazi, au gari la farasi, wengine walipanda mgongo wa mnyama, na wengine walitembea kwa miguu.

³⁹ Na wakati ulipokuwa ukitembea, mbona, walikuwa na vazi lisilokaza, kitu kama joho, linalopwaya, na chini ya vazi hilo walikuwa na vazi la ndani. Kwa sababu kutembea, na kadhalika,

hilo vazi linalopwaya. . .Ndipo unapofika kwenye nyumba ya mgeni, ulipoalikwa. . .

⁴⁰ Mnasikia ambapo kanisa, bado, tunafanya hivyo kanisani mwetu, tunaadhimisha kutawadha Miguu. Sasa, wao wanasema ni mapokeo, bali hata hivyo ni—ni amri. Wanasema walifanya hivyo wakati huo kama mapokeo, nao kweli walifanya, lakini Yesu alikuacha kama mfano, na basi kama alifanya hivyo, ni amri. Kwa hiyo basi sisi, wakati. . .

⁴¹ Mtu aliyelipwa mshahara mdogo kuliko wote kazini alikuwa ni yule waliyemwita mwosha miguu, kwa kweli alikuwa ni mtumishi tu, alipata pesa ki—kidogo sana kuliko wote, kwa sababu nyumbani aliwatawadha tu wageni miguu walipoingia.

⁴² Ndipo ninamwazia Bwana wetu! Wakati mwingine tunafikiri kwamba sisi ni mtu *muhimu*, wakati Mungu wa Mbinguni alipobadilisha hadhi Yake kutoka kwa Mungu akawa mwanadamu, kisha akachukua nafasi, si ya mfalme, bali mtumishi mwosha miguu kuwatawadha wanafunzi Wake miguu, na kuipangusa kwa kile kitambaa alichojifunga. Ndipo ikiwa hatuna heshima iliyo kubwa sana tunapokaribishwa, ama, tunapotaka kukaribishwa! Hatuna budi kuangaliwa na kila mtu. Ndipo ninawazia juu ya Bwana wetu, jinsi alivyotupa mfano wa kuchukua mahali pa chini sana palipokuwapo, kutawadha miguu ya wageni.

⁴³ Na sasa, miguu yao ilichafuka walipokuwa wakitembea, kwa sababu walikuwa na makubadhi, kitu kama yale makubadhi ya Kirumi wanayovaa siku hizi, ambayo yalihesabiwa kuwa viatu vyao, na kisha pia, juu ya viungo vyao, kwa kuwa vazi la ndani lilipanda juu. Na wakati lile jo—joho likipeperuka kwenye vijia vinavyopanda juu ya milima. . .

⁴⁴ Hawakuwa na barabara pana kama tulizo nazo leo, wanyama walipitia njia hizi pia, ngamia, na nyumbu, farasi, na njia mbalimbali za usafiri. Na njiani kukajaa mavumbi, na—na uvundo mavumbini.

⁴⁵ Basi walipokuwa wakitembea katika mavumbi haya, vazi hilo lililokuwa likifagia mavumbini liliokota uchafu. Basi wakati walipokuwa wakitokwa na jasho, ambapo joto la jua la Palestina ni kali sana, basi jasho lao likawa, likanata, nayo harufu hii ya farasi, na wanyama barabarani, waliokota mavumbi haya nayo yakawashika, wa—wanguka vibaya, kwa sababu kwamba walikuwa wakitembea, huku mavumbi haya yakiwashika.

⁴⁶ Basi ulipomwalika mgeni nyumbani kwako, jambo la kwanza lililotukia kumkaribisha mgeni huyu, baada ya huo mwaliko, kwanza ilibidi waalikwe, na kisha, kabla hawajajisikia nyumbani kweli, iliwabidi watayarishwe kwa ajili ya hilo.

⁴⁷ Laiti ningalikuwa na wakati wa kueleza yaliyo moyoni mwangu kutuhusu sisi tunapokuwa na uamsho. Tunamwalika

Yeye, lakini nashangaa kama tunamshughulikia akiisha kuja, ama tunamsukuma kando?

⁴⁸ Ndipo m—mtumishi mtawadha miguu, kama vile ningemwita, wakati mtu alipokuja mlangoni huyo ndiye mtu wa kwanza kukutana naye, kwa sababu a—alikuwa, hakunukia vizuri, amejaa mavumbi. Kwa hiyo jambo la kwanza walilofanya lilikuwa ni kuvua viatu vyake, kumwosha vikanyagio na miguu, kisha akachukua makubadhi yake na kuyaandaa, na kumpa jozi ndogo ya kitu kama sapatu, kitambaa kidogo alichoweka juu ya miguu yake, kutembea juu ya mazulia mazuri ya kutoka ng'ambo ya nyumba za hawa matajiri.

⁴⁹ Halafu jambo la pili walilofanya, baada ya huyo mtumishi mtawadha miguu, basi alinyosha mkono kwenye rafu na akachukua manukato. Na wakati mwingine haya ni ghali sana, sana. Ndipo huyo mgeni akanyosha mikono yake, naye akammiminia manukato mkononi mwake, akaosha mikono yake, kisha akayapaka shingoni mwake, akaosha uso wake na ndevu zake, kisha akachukua ta—taulo, akajipangusa, na wakati mwingine shingo yao ilikuwa inawaka moto.

⁵⁰ Basi manukato haya fulani yalitokana na uvumba wa kifalme, wa gharama kubwa (watu matajiri walikuwa nao). Wanadai kwamba baadhi yake hata yalikuwa ni baadhi ya yale malkia wa Sheba aliyomletea Sulemani. Yanapatikana huko juu kabisa milimani, kwa nadra sana, wanayatengeneza kwa chipukizi dogo la waridi, ambalo huwa tofaa. Nao inawabidi kupanda juu, nayo manukato haya hutengenezwa kwa nadra sana ambayo matajiri hutumia ku—kuwapaka wageni wao wanapoingia.

⁵¹ Ndipo basi, wakachukua taulo na kupangusa uso wake, ndipo shingo yake basi ingejisikia baridi, na miguu yake ilikuwa safi, naye alikuwa amepumzika. Alijisikia zaidi kukutana na bwana wa nyumba. Kisha akaenda kwenye chumba cha pili, na ni nani aliyesimama pale, ila mwenye nyumba.

⁵² Ndipo ikawa... Wangekutana nao (Simama kwa dakika moja tu, Ndugu.) kitu kama hiki: Wakati mgeni huyo alipoingia, sasa, asingejisikia kukutana na bwana wa nyumba kama alikuwa, miguu yake ilikuwa michafu, nao mwili wake ulikuwa ukinuka kwa ninii, ukinuka kama wanyama ambao wamepitia hiyo njia, na miguu yake yote inauma na imejaa mavumbi, na shingo yake ikiuma sana. Angeweza, baada ya kuoshwa, na—na alikuwa, harufu mbaya ilikuwa imemtoka, na ninii, alikuwa amepakwa manukato na ni safi, angekutana na mwenye nyumba.

⁵³ Ndipo basi wangeweka mikono yao, na kupigapigana *hivi*. Ndipo walipofanya hivyo, walisalimiana kwa busu pande zote mbili za shingo, mnaona, kwa hiyo basi wao (Hebu simama kidogo.), namna *hii*, wakabusiana pande zote mbili za shingo.

(Samahani. Ilinipasa kuwa nimemalizana na hayo maonyesho mengine.) Basi akiisha kuoshwa na kupakwa manukato, shingo yake haina mavumbi juu yake, haina harufu ya samadi, lakini manukato yake yalikuwa pale, basi, alijisikia safi, ili kwamba yu—yule aliyekuwa amemwalika angejisikia *huru* kumbusu shingoni.

⁵⁴ Ndipo alipombusu, hilo busu lilikuwa ni makaribisho: “Karibu ndani, kila kitu, jisikie tu nyumbani,” wakati alipombusu na kumsalimia, “ingia, kila kitu ni chako, wewe ni mmoja wetu sasa, miguu yako imeoshwa, na u—umepakwa manukato, na kupambwa, na sasa nimekukaribisha kwa busu, sasa, ingia tu nyumbani kwangu, na uende tu kwenye friji na upate chakula, ujilaze chini, fanya lolote utakalo, uko tu nyumbani sasa, kwa sababu nimekukaribisha.”

⁵⁵ Huyo mtumishi mtawadha miguu alimpitaje? Laiti ningalikuwa huko, ni—ni—ningekuwa nikimtazamia. Ngingekuwa na karai maalum ya maji tayari kwa ajili Yake. Ningelipenda kukutana Naye. Sijui, hapana shaka jambo fulani lilitukia, ha—hakuwa pale, alimkosa. Wala hakuna aliyembusu, hakuna aliyemwosha, hakuna aliyempamba, hakuna aliyemkaribisha, bali Yeye alikuja kwa vyovyote vile, kwa sababu alikuwa amevalikwa.

⁵⁶ Nashangaa, wakati mwingine tunapomwalika, je, tunawazia mambo hayo? Mkaribishe, usimwonee haya. Mara tu anapoingia moyoni mwako, mwabudu Yeye. “Bwana, njoo moyoni mwangu,” basi ajapo, je, unaona aibu, kwa sababu umesimama mbele ya mtu mwingine? Unapomsikia mtu akilitaja bure Jina Lake la thamani, unaona aibu kwenda na kusema, “Usifanye hivyo, hilo linaniudhi sana, Huyo ni Bwana wangu, ni kwamba unalitaja Jina Lake bure.” Sijui kama kweli tunamkaribisha? Natumaini tunafanya hivyo.

⁵⁷ Kuna wengi sana siku hizi, watakaomwalika mjini kwa ajili ya uamsho, na ndipo Yeye anaweza kuja, halafu wanasema tu, “Loo, achana na upuuzi huo, ni bure.” Tunamwalika, bali kamwe hatumkaribishi. Wakati mwingine, labda, tunafikiri Yeye angesema jambo fulani kinyume na imani yetu.

⁵⁸ Kwa nini Simoni hakumkaribisha? Kwa nini hakumjali? Walimkosaje? Lakini Huyo hapo ameketi pembeni, kama tu ua la ukutani, maskini kichwa Chake cha thamani, kikiinama chini, kila mtu akipita. Loo, walivutiwa na hayo mambo, naye mchungaji alikuwa pale, nao walikuwa na mikusanyiko yao ya kijamii na gumzo lao, lakini vipi kuhusu maskini Yesu? Mbona, Yeye hakukaribishwa, Yeye . . . hakuna mtu . . . Mbona, ha—hata miguu Yake haikuoshwa. Kulikuwa na uvundo, Yeye hakupendeka, hakukaribishwa.

⁵⁹ Nami nashangaa, wakati mwingine, katika njia hii kuu, nzuri tunayoita utakatifu, utamu, sijui kama maisha, wakati

mwingine, tunayowaonyesha watu hayamfanyi kidogo tu asiye karibishwa, pia, kwa sababu ya tabia yetu, kwamba hatuishi sawasawa kabisa, mtu afaaye kumwakilisha Yeye, kughairi, na kukwepa, na msimamo dhaifu *huku* na *kule*. Kama amekuja nyumbani kwetu, tunapaswa kushukuru, Mgeni yule wa Galilaya.

⁶⁰ Lakini Huyu hapo, ameketi kwenye kona, hata hivyo akiacha ratiba Yake yenye shughuli nyingi, Naye alikuwa papo hapo kwa wakati ufaao. Yesu kamwe hakosi miadi, Yeye huitimiza yote, unaweza kutegemea hilo. Anapofanya miadi, Yeye yuko pale kuitimiza.

⁶¹ Na kuna miadi moja ambayo sote tutaikabili, kwa sababu Yeye ameifanya pamoja nasi sote, hiyo ni kwenye ile Hukumu. Yeye atakuwepo, na wewe pia, sote tutasimama pale.

⁶² Lakini huyu hapa kwenye kona. Ninapowazia jambo hilo wakati mwingine linaufanya moyo wangu ujisikie kigeni, nafikiri, “Yesu, akiketi pembeni, akiwa na miguu michafu.” Kama vile Mfaransa anavyomwita: *Jésus. Jèsus* akiwa na miguu michafu. Linasikika la kukufuru, bali hivyo ndivyo alivyokuwa, hivyo ndivyo walivyomwacha, hivyo ndivyo walivyomwacha aketi: akiwa na miguu michafu. Mgeni mwenye heshima, alivyodhaniwa kuwa, nao walikuwa na shughuli nyingi *sana* na kazi zao, mpaka Yesu akaketi na miguu michafu. Sijui kama hatuvutiwi sana siku hizi katika kuona kwamba kundi letu linakua kubwa kuliko hilo lingine, hata tusimwache ameketi vivyo hivyo. Lakini Yesu, akiwa na miguu michafu, hajakaribishwa.

⁶³ Kulikuwako na maskini mwanamke mmoja katika mji huo aliyejipatia riziki kwa njia mbaya sana, alikuwa ni mwanamke wa—wa danguroni, ninii, ukahaba, mnaelewa. Na labda alikuwa amechelewa kidogo asubuhi hiyo kuingia mtaani. Basi aka hesabu maskini dinari zake za Kirumi alizokuwa akiweka akiba, labda apate kujinunulia nguo nzuri zaidi siku moja. Na jinsi alivyopata pesa zake ilikuwa ni kwa sifa mbaya.

⁶⁴ Alikuwa na jina baya miongoni mwa watu, hata hivyo hebu tuwazie yeye alikuwa tu ni msichana aliyekuwa amefanywa kwenda mtaani, si kwa sababu alikuwa mhalifu, labda, bali kwa sababu alikuwa na wazazi wahalifu, hawakujaribu kumtunza. Hiyo ndiyo sababu wengi wao wako mtaani siku hizi: Sio uhalifu wa watoto, ni uhalifu wa wazazi.

⁶⁵ Nilikuwa nikisikia asubuhi ya leo nilipotoka chumbani mwangu, ya kwamba watoto wadogo watano waliangamia Chicago jana usiku katika moto, kwa sababu mama mmoja alimwacha msichana tineja mdogo alinde, ndipo hiyo nyumba ikateketea, ikawateketeza watoto wake, akiwa huko nje kwenye karamu mahali fulani.

⁶⁶ Mimi na mke wangu tulikuwa tukipitia mtaani jana, na kuona yapata watoto wadogo wanne wameketi kwenye gari, huku maskini msichana mwenye umri mkubwa zaidi hakuwa amezidi umri wa yapata miaka saba, akiwa na mtoto mchanga wa kunyonya. Mmoja wa hao wavulana wadogo alitaka kuambatana na Mama yake, naye mama akatoka kwenye gari, na kuwasha sigara, kisha akafunga mlango kwa nguvu, kasema, “Wewe keti humo,” naye huyo akaingia katikati ya mji, akaingia kwenye baa. Na ni mtoto mwenye umri wa miaka saba, kwenye mitaa ya Chicago, mtaa wenye shughuli nyingi sana, Lincoln ya chini, nao pale wameketi pale kwenye gari lile pamoja na mtoto mchanga, mtoto mchanga wa kunyonya, huku upepo huo ukivuma kwa nguvu sana nusura nigande, mimi mwenyewe. Sijui, wakati mwingine nafikiri ni kosa la mzazi.

⁶⁷ Labda maskini msichana huyu alilelewa katika nyumba kama hiyo, naye alikuwa tu ameachiwa kwenda mtaani. Angalikuwa na mama mwombaji, kama huyu ndugu mlevi sugu alivyokuwa naye, huenda mambo yakawa tofauti, alisema mama yake alikuwa amemwomba.

⁶⁸ Hebu niseme hivi: Wakati yule Mrumi alipoongoka, Paulo...yule mlinzi wa gereza la Filipi, huko Filipi, alisema, “Nifanye nini nipate kuokoka?” Wengi wetu tungemwambia yale asiyopaswa kufanya: aache kunywa pombe, aache kuiba, aache kusema uongo, aache kuvuta sigara. Lakini hilo halikuwa swali lake, “*Nifanye nini?*”

Paulo akasema, “Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe pamoja na nyumba yako mtaokolewa.”

⁶⁹ Unasema, “Mtu anapookoka, je, hiyo huiokoa nyumba yake?” La, lakini kama ana imani ya kutosha kuokoka mwenyewe, ana imani ya kutosha kwamba nyumba yake itaokolewa pia, imani ile ile iliyomwoko. Hivyo ndivyo yule mama alivyowazia, kaburini muda mrefu uliopita, lakini maombi yake yalijibiwa tu.

⁷⁰ Mama mhalifu na baba mhalifu hufanya mtoto mhalifu. Labda, hebu tuseme, maskini msichana huyu alikuwa na baba na mama ambao hawakumjali, naye akaingia mtaani katika umati mbaya. Alipofanya hivyo, alitengwa, hakuna mtu aliyemjali.

⁷¹ Maskini mhubiri huyu aliyeketi hapa, akiandika muhtasari huu sasa, wakati alipokuwa akiniambia, ya kwamba alikuwa na yapata pembe arobaini hapa Chicago alizohubiria, ama kuwatumia watu kuhubiri, Mungu ambariki mvulana huyo. Tupe hao wa mikutano ya mitaani, hivyo ndivyo unavyowaingiza hawa walevi na kadhalika. Baadhi yetu hupanda juu sana na ni watu wa hali ya juu sana tusiweze kusimama pembeni tena, kuingia kwenye vitongoji duni. Yesu alisema, “Enendeni kwenye mipaka, na njia kuu, kila mahali, washurutisheni; saa imekaribia.”

⁷² Lakini jinsi, labda, katika siku hizo hawakuwa na mmoja mtaani, huko chini katika mji wake. Lakini akatoka nje, baada ya kuufunga mlango, kisha akashuka kwenye vipandio vidogo, vinavyokereza nyuma kwenye kichocho, na kutoka nje, akajipamba apate kukutana na umma, na, apate pesa zaidi kote katika siku, kwa njia yake ya kujipatia riziki. Na jambo la ajabu lilikuwa, hapakuwapo na mtu mtaani, kila mtu alionekana kuondoka. Kwa hiyo wakati akipita mtaani, mbona, alishangaa, “Ni likizo ya aina gani hii? Kuna shida gani? Watu wote wameondoka kwa sababu fulani.”

⁷³ Ndipo akasikia harufu nzuri ya huyo mwana-kondoo aliyechomwa ikipitia hewani, na labda hakuwa amekula kwa siku chache, akijaribu kuweka akiba baadhi ya pesa zake ajinunulie nguo yake nzuri. Akasikia harufu hiyo nzuri, naye akasema, “Loo, hapana shaka mtu fulani ana ka—karamu inayoendelea.” Naye akaifuata mpaka akakaribia. Na nje ya mihimili ya lile jumba kubwa, zuri ambalo Simoni aliishi, mahali ambapo, karamu ilikuwa ikiendelea, watu maskini walikuwa wamesimama pale, *wakinusanusa*, wakivuta harufu nzuri na kuramba midomo yao. Nao matajiri walikuwa mle ndani, wakinywa divai, na kujiandaa kwa ajili ya chakula chao cha kutwa.

⁷⁴ Ndipo maskini mwanamke huyu akajipenyeza akaingia, basi wakati wangemwona akija, bila shaka wangerudi nyuma, kwa sababu alikuwa mwenye sifa mbaya. Ndipo hatimaye akapanda juu, mpaka akaweza kuchungulia ndani ya miimo, aone kama angeweza tu kupata ku—kukiona kitu hicho, kilichokuwa kikitoa hiyo harufu ya kuridhisha, kuangalia lile jiko la nyama choma kuona jinsi mwana-kondoo alivyokuwa akichomwa, na kuwazia tu kwamba wakati mmoja maishani mwake huenda akaketi kwenye mlo mzuri. Na labda alishika nywele zake nzuri na kuzitengeneza zote, mwajua, kwa kuwa alikuwa huko nje mtaani.

⁷⁵ Naye alipoangalia kote kwenye wasikilizaji, alimwona Simoni Farisayo amesimama pale, akitoa hotuba zake mbele ya watu mashuhuri wa mji huo, huyu hapa Daktari, Ph.D., LL.D. Jones, na mchungaji, na huyu hapa msaidizi wake, na hawa hapa watu wote mashuhuri kutoka kwenye miji mbalimbali, wamesimama pale, mwajua, *halisi* na wenye heshima.

⁷⁶ Akawaza, “Loo, angalia kule, jinsi matajiri walivyo na yote!” Akiangalia kote, akawaza, “Vema, nitakwambia, ni... daima wanaalika, bila shaka, wale, tabaka lao wenyewe, nasi kamwe hatuna nafasi.”

⁷⁷ Lakini baada ya kitambo kidogo macho yake yakaelekea pembeni, hapo ameketi maskini Mtu asiyetambulika. Naye angeweza kujua ya kwamba alijaa mavumbi, “Vema, aliingiaje mle? Sijui huyo ni Nani.” Alikuwa ameinamisha kichwa Chake,

hakuna mtu aliyekuwa akimjali. Akawaza, “Vema, sijui jinsi alivyopata kuingia. Mbona, hapana shaka aliingia kisiri bila kualikwa. Miguu Yake haijaoshwa, utu Wa—Wa—Wake, uso Wake haujapambwa. Hakuna mtu anayemjali. Sijui ni kwa nini.”

⁷⁸ Naye alipokuwa akiangalia, Yeye akainua kichwa Chake, macho yake yakakutana na Yake. Mnajua hilo linapotukia, jambo *fulani* linaendelea. Akamtazama usoni, akasema, “Sijapata kumwona mtu yeyote *akionekana* tu namna hiyo. Sijui Huyo angeweza kuwa ni Nani. Nashangaa!” Na labda, mtu fulani aliyesimama karibu. Akasema, “Kwa nini Mtu huyo ameketi pale?”

Vema, huyu hapa mmoja wa, wafuasi wa kanisa la Simoni ndiyo kwanza aje, kwa hiyo huenda alisema . . .

“Mbona yule . . .?”

“Loo, hivi huelewi? Tutakuwa na burudani, leo, kutoka kwake. Simoni, bwana wetu, alimwalika hapa. Unajua huyo ni nani?”

“La. Nashangaa.”

“Loo, huyo ni yule nabii wa Galilaya, aitwaye Yesu wa Nazareti.”

Basi Jina hilo lilipougusa moyo wa maskini kahaba huyo, alisema, “Ati Yesu wa Nazareti?”

“Naam.”

⁷⁹ Basi akaangalia nyuma kwenye kona, na huyo hapo Yeye ameketi, ndipo akasema, “Loo, kuwazia kwamba Yeye amealikwa, Naye hajapambwa, wala miguu Yake haijaoshwa! Ninakumbuka kwamba wananiambia ya kwamba mwanamke fulani alikokotwa mtaani, ama, aliburutwa mtaani kwa sababu ya ukahaba, apate kupigwa mawe kama vile ni—ningepigwa, Naye akamsamehe kila dhambi. Laiti ningaliweza tu kumfanyia jambo fulani, labda Yeye angenisamehe dhambi zangu. Lakini nifanye nini? Hata siwezi kuingia malangoni. Laiti ningaliweza tu kumfikia, ningetaka kumwomba anisamehe.”

⁸⁰ Kwa hiyo akawazia, “Yeye hajapakwa mafuta, wala hajaoshwa, wala hajakaribishwa. Laiti ningalipata tu usikivu Wake, ningemkaribisha. Laiti angezungumza tu nami, ningemkaribisha.”

⁸¹ Kwa hiyo anageuka, na kuingia moja kwa moja mtaani, chini, juu ya vile vipandio vidogo, vinavyoalika huko nyuma. Akawazia jambo fulani, akanyosha mkono kwenye soksi yake aliyokuwa ameifungia, naye akachukua vipande hivi vya fedha za Kirumi, ndipo akawazia, “Loo, siwezi kufanya hivi. Kama nikienda na kununua kibweta hiki, mbona, Yeye angejua hasa jinsi nilivyopata pesa hizo, kwa sababu wananiambia Yeye ni Masihi, nami ninaamini hilo, na endapo Yeye ni Masihi, atajua ya kwamba mimi ni mtu mbaya.”

⁸² Ndipo akaziokota zile pesa na kuanza kuzirudisha kwenye sanduku, lakini Kitu fulani kikasema, “Hii ndiyo nafasi yako, huenda usiipate tena.”

⁸³ Kwa hiyo ni somo: Kamwe usiikatae nafasi hiyo ya kwanza ambayo ungeweza kukutana Naye. Haidhuru itagharimu nini, kwamba inakubidi kukiri makosa kiasi gani, fanya hivyo sasa, kwa sababu zitajulikana kwenye ile Hukumu kwa vyovyote vile.

⁸⁴ Akachukua fedha kidogo alizokuwa akiweka akiba, akasema, “Lakini hizi ndizo zote nilizo nazo, lakini inaleta tofauti gani, maadamu ninaweza kumfikia Yeye!”

⁸⁵ Huyu akashuka mtaani, naye anaingia kwenye duka la manukato, na hapa huyu naye anajitokeza humo, asingeweza kuondoka kwenda karamuni, bila shaka, kwa sababu alidhani angekosa mauzo mahali fulani. Mwajua, yule aliyesema, “Ina faida gani, kama tukimwacha Yusufu shi—shimoni hapa? Hima tumwuze, tupate pesa kwake.”

⁸⁶ Akatokea, akagonga kaunta, naye akatoka akaona ilikuwa ni kitu gani, akaanza kugeuka, lakini mwanamke akamwaga dinari hizi za Kirumi kwenye... Loo, hakika, pesa, mtu yeyote anaweza kuingia sasa. Hakumtaka mahali pake pa biashara, mpaka alipoona kwamba alikuwa na pesa, basi wakati alipokuwa na pesa, loo, vema, hiyo ni tofauti, mnaona, “Unataka nini?”

⁸⁷ “Ninataka yaliyo bora kuliko yote uliyo nayo. Ninataka, sio tu kibweta cha kawaida cha *manukato* haya, ninataka yaliyo bora kuliko yote uliyo nayo kwenye kaunta. Ni kwa ajili ya tukio maalum.” Hicho ndicho unachopaswa kumpa Yesu. Chukua nafasi yako ya kwanza kumwendea, na kumpa kilicho bora kuliko vyote. Mpe moyo wako, mpe yote uliyo nayo, kwa kuwa huenda asipite huku tena, hebu na tufanye yote tuwezayo kwa ajili Yake wakati tuwezapo.

⁸⁸ Anaweka hicho kibweta chini ya mkono wake, naye huyo anapanda kwenda barabarani, basi akafika kwenye hivyo vizuizi, na yule pale Yesu akiwa na miguu michafu, angali ameketi, hakuna mtu anayemjali, akawaza, “Ninawezaje kuingia?”

⁸⁹ Baada ya... Dakika chache tu kabla ya kutakiana heri, na divai nzuri za kupendeza zilizonywewa, na kadhalika, hapana shaka aliona yule mtumishi mtawadha miguu ameondoka, kwa hiyo akaingia kisiri, akajipenyeza huko nyuma. Mwajua, kuna jambo fulani kulihusu, kama ukipata kumtazama, utafanya lolote kumfikia, sijali ni nini. Inakubidi kujipenyeza chini ya upande wa nyuma ya hema ama chochote kile, utafanya jambo fulani kumfikia, kama akikuangalia machoni, nawe unaweza kuona Yeye ni Nani.

⁹⁰ Naye anaingia kisiri kwa njia ya nyuma, kisha anajipenyeza kupitia kwenye umati, kumzuia mtu yeyote... maana alikuwa,

alikuwa na jina baya. Mbona, Simoni angalimfanya arushwe juu ya ua, kwa hiyo, lakini alikuwa amedhamiria, haidhuru, atajitahidi kwa vyovyote vile.

⁹¹ Wakati mwingine kanisa linaweza kuwazia kama ukishuka uende miongoni mwa kundi hili la watakatifu wanaojibingirisha, kwamba utatupwa nje ya mlango. Vema, inaleta tofauti gani? Mradi tu utafika kwa Yesu, hilo ndilo jambo muhimu, hilo ndilo jambo muhimu.

⁹² Akashuka akaja karibu na upande huo, kando ya huo ukuta, na Yeye huyu hapa ameketi pale ameinamisha kichwa Chake, nywele Zake zimejaa mavumbi, na uso Wa—Wake wote imejaa mavumbi, ndevu Zake zimejaa mavumbi, miguu Yake imevalishwa maskini makubadhi Yake ya kutembelea, viungo vyake vimejaa mavumbi na vinanuka. Ninaweza kumwona akianguka miguuni Pake. Alikuwa kwa njia sahihi, akaanguka miguuni Pake.

⁹³ Akamwangalia, akaogopa, akawazia, “Vi—vipi kama Yeye—vipi kama akisema, ‘U nani wewe? Unafanya nini hapa?’” Lakini ninaweza tu kumwona akiunyosha mguu Wake. Alijua alikuwa anakuja.

⁹⁴ Akasema, “Loo, kama a—kama akiniangalia na kujua mimi ni kahaba!” Anajua hilo kwa vyovyote vile. “Lakini ningetaka kumfanya jambo fulani. Ningependa kumwonyesha shukrani zangu, kwa sababu ninaamini Yeye ni Mungu. Nami ninataka kuonyesha jambo fulani, shukrani kidogo.”

⁹⁵ Ndipo alipomtazama Yeye, Naye akatazama, alijua ya kwamba alikuwa miguuni pa Yesu, yale machozi makubwa mno yakaanza kutiririka mashavuni mwake. Akampigapiga miguuni. Alikuwa miguuni pa Bwana wake. Akaanza kupigapiga miguu Yake, ndipo machozi makubwa mno ya toba yakaanza kububujika, yakidondokea miguuni Mwake. Alishukuru sana kuwa miguuni Pake.

⁹⁶ Basi akaangalia, nayo miguu Yake ilikuwa imelowa machozi yake, alikuwa akilia huku ameinamisha kichwa chake, nywele za—zake nzuri za mawimbiwimbi hapana shaka zaliangukia pande zote namna *hii*, hakuwa na taulo, nazo nguo zake zilikuwa chafu sana, labda, kuiosha ninii Yake, ama, kuipangusa miguu Yake, kwa hiyo alizishika tu nywele zake na kuanza kumtawadha miguu, na *kubusu*, *kubusu* kuibusu miguu Yake; alikuwa na shukrani. Loo, jinsi tunavyopaswa kujisikia vivyo hivyo! Sio kujigamba.

⁹⁷ Wengi wa dada zetu wa Kipentekoste ingewabidi kusimama kwa vichwa vyao kufanya hivyo, tayari wamekata nywele zao. Lakini nywele zake, alikuwa akiosha miguu Yake, akiibusu. Loo, alikuwa miguuni pa Bwana wake, akiibusu miguu Yake.

⁹⁸ Basi baada ya kitambo kidogo Simoni akageuka na kuangalia, “*Hmm!*” Jamani, uso wake umejaa hasira, na...

“Sasa, angalia kilicho nyumbani mwangu! Nilimwalika huyu mtakatifu anayejibingirisha hapa, basi angalieni kile, tabaka la—lake mwenyewe limekuja, hao hapo watu wa tabaka moja.” Wangali wana wazo lile lile, nina furaha sana.

⁹⁹ Ninataka...ningetaka niwe na machozi ya kuosha...Ni maji mazuri jinsi gani: machozi ya toba yakiosha miguu ya Yesu, machozi yakitiririka kutoka mashavuni mwa mwanamke mwenye sifa mbaya, yakitawadha miguu ya Yesu. Maji matamu kuliko yote aliyowahi kuwa nayo, yaliyopata kuosha miguu Yake, machozi ya toba yakitiririka miguuni mwa Yesu.

¹⁰⁰ Huyu kijana mwanamke mrembo anayeketi pale. Simoni akageuka, ananong’onezea dhehebu lake, kasema, “Mnaona? Hiyo inaonyesha yeye ni nabii wa jinsi gani. Kama mtu huyo angekuwa ni nabii, angejua ni mwanamke wa aina gani aliyekuwa akiitawadha miguu Yake.” Maskini mnafiki we! Unafikiri Yeye hakujuu hilo? Kasema, “Mnaona, niliwaambia yeye hakuwa nabii.”

¹⁰¹ Mnaona, walikuwa na wazo lao wenyewe kuhusu dini, walikuwa na wazo lao wenyewe kumhusu Mungu, bali lilikuwa maili milioni moja kutoka kwenye kitu kilicho halisi. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi: “Tuna kanuni zetu za imani tulizojiundia wenyewe na mawazo yetu juu yake. Maadamu sisi ni Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, ama Wapentekoste, ni sawa.” Lakini kwangu mimi, nitachukua machozi ya toba. Niyachukue maisha yangu na yote niliyo nayo, kusaidia kuliosha hilo jina chafu la mtakatifu anayejibingirisha kutoka kwa yule Bwana Yesu halisi, yule Mwana wa kweli wa Mungu. Yeye anawaziwa siku hizi kuwa mlokole fulani wa dini, telepathia, ama mtu aliyechanganyikiwa kiakili.

¹⁰² Nijalie maishani mwangu, nimwage si machozi yangu tu bali moyo wangu, na yote yaliyo ndani yangu, nisimame na kujaribu kuishia yaliyo mema kwa neema Yake, kamwe nisipatane juu ya Injili hiyo nzuri, yule Roho Mtakatifu aliyeniokoa. Mwrite vyovyote utakavyo, kwangu mimi, ni Yesu. Nao ulimwengu unamwacha aketi akiwa na miguu michafu, akiwa na jina chafu kama *mtakatifu anayejifingirisha*, mtu mwenye nia ya uhalifu, ama kitu fulani ndicho cha pekee alichochacho, hivyo ndivyo wanavyowazia.

¹⁰³ Simoni, mwekundu usoni, “Ha! Angalieni hapa, tulimleta huyu mtakatifu anayejifingirisha hapa tupate baadhi, tuliwazia tungepata burudani kutoka kwake, ningethibitisha ya kwamba yeye hakuwa nabii. Anajiita *nabii*, yeye ni mwanatelepathia tu. Yeye amepagawa tu na ibilisi, yeye ni mpiga ramli. Na hilo linathibitisha hoja yangu, huyo hapo, ameketi pale kwenye kona, na wa aina yake pamoja naye. Na hapo mwanamke huyu mwenye sifa mbaya, amesimama pale, akiitawadha miguu Yake.”

¹⁰⁴ Labda yule mtumishi mtawadha miguu aliagizwa asiitawadhe miguu Yake, kusudi tu wapate onyesho fulani kutoka Kwake. Watu wengi huja kwenye mikutano yetu kucheka tu, wanafikiri wanaweza kupata burudani kutoka Kwake. Anajua moyo wako, utasimama mbele Zake siku moja, ewe mwenye dhambi.

¹⁰⁵ Hapa hivi majuzi kundi la watu lilikusanyika huko nyuma, wahudumu wanafunzi, na kila wakati ningeanza kuhubiri, wangesema, “Haleluya, Bwana asifiwe, haleluya,” bila kujua ya kwamba Mungu yuyo huyo wanayemdhihaki, atakuwa Hakimu wao siku moja. Vema.

¹⁰⁶ Lakini akaendelea, haidhuru Simoni alisema nini. Sasa, Simoni akisafisha koo lake, na mwekundu usoni, huku hasira yake ya haki imepanda, naye akiwa tayari kulipuka, alivutia usikivu wa watu wote, alipogeuka na kujinyosha, “*Hmm!*” Farisayo anayejiona mwenye haki, mnafiki, mfuasi wa kanisa, huyo ndiye laghai mbaya sana nimjuaye, ni maskini mwaminio mwenye mgongo wa kuvumwani. Yeye ni katili kuliko makahaba wote na matineja laghai walioko nchini, atawapeleka watu mbali na Mungu kuliko chochote kile, kila baa iliyopo mtaani.

¹⁰⁷ Huyo hapo ameketi pale. Ndipo akasimama, na kuchukua kile kibweta, na kujaribu kukivunja. Ana wasiwasi sasa, kwa sababu anapoangalia juu, Yeye anamtazama moja kwa moja. Usijali, Yeye anakuangalia, pia, Yeye anakuangalia sasa hivi. Tunaweza tu kuhisi Uwepo Wake unaochoma. Alikuwa na wasiwasi, alijaribu ku—kufungua kifuniko kwa nguvu, alifungua tu hicho kifuniko kwa nguvu, kisha akayamiminia tu kichwani Mwake, akaanza kumtia mafuta.

¹⁰⁸ Loo, umati wote unatazama, “Naam, angalieni pale. Huyo hapo, hatukuwahi kumwona hapo kabla, ameketi pembeni, kahaba akiwa karibu naye.”

¹⁰⁹ Ninaweza kumsikia Simoni akisema, “Hivi niliwaambia? Uh-huh. Huyo hapo nabii wenu, huyo—huyo hapo. Mnaona? Angejua alikuwa akishirikiana na umati wa aina gani.”

¹¹⁰ Loo, ni mara ngapi nimetupiwa hayo usoni mwangu! “Ndugu Branham, kama karama hiyo ilikuwa ni ya Mungu, usingekuwa pamoja na kundi hilo la Wapentekoste.” Hao ndio wanaoipokea, hao ndio wanaoiamini.

¹¹¹ Hivi majuzi nilikuwa nikizungumza na mtu kutoka kanisa la Kimethodisti, alikuja kujiandikia tasnifu juu ya uponyaji wa Kiungu, akasema, “Kwa nini usije kwenye kanisa la Methodisti?”

Nikasema, “Kwa nini usinalike?” Nikasema . . .

Akasema, “Mimi ni mchungaji.”

Nikasema, “Vema, wakusanye mashemasi wako, na halmashauri yako pamoja, na mzee wenu wa jimbo, na wote pamoja, tuone kama watanalika.”

Akasema, “Loo, hawatafanya hivyo, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Hivyo ndivyo nilivyowazia.”

Akasema, “Jambo pekee wanaloweza kushikilia dhidi yako ni kwamba wewe ni Mpentekoste, uliliacha kanisa la Baptisti ukawa Mpentekoste.”

¹¹² Nikasema, “Hao ndio wanaoipokea.” Hiyo ni kweli. Hao ndio walio tayari kuipangusa miguu michafu ya Yesu, kulitetea Jina la Yesu, ile shutuma.

¹¹³ “Hapo, kama alikuwa ni nabii, angefahamu anashirikiana na mtu wa aina gani.”

¹¹⁴ Kwa hiyo sasa anaogopa anapomwona kila mtu, kimya kitupu kinaingia, na kila mtu amesimama akiangalia. Ninaweza kuwaona wanawake wa chama, mwajua, wametoa hiyo miwani namna *hii*, mwajua, watu wote mashuhuri wamesimama, wakiangalia, mwajua, huku wamenyosha shingo zao. Yesu bila kuwajali, Yeye anaangalia ni nani anayemtumikia. Yeye hajali una Ph.D. ngapi, ama LL. D, Yeye hajali kanisa lako ni la jamii gani mjini, anataka kumpata mtu atakayemtumikia.

¹¹⁵ Wawe ni weupe au weusi, wa manjano, hudhurungi, maskini au matajiri, wafungwa au walio huru, wa kiume au wa kike, Yeye anataka mtu atakayemtumikia. Yeye yuko katika...Huduma Yake ni hitaji siku hizi, inahitaji kuoshwa. Yeye hajali tuna madhehebu mangapi, tunawainua watu wangapi mashuhuri, tunajenga shule ngapi, anataka mtu fulani amtumikie, mtu ambaye ataishi hayo maisha, mtu atakayeshuhudia kuwa na Roho Mtakatifu, kuishi maisha yasiyo na lawama, hiyo ni kweli, mtu wa kuishi maisha yanayoweza kuzaa. Nao wanaongea juu ya Yesu, kisha wanamzaa Yesu. Mtu atakayesaidia kuosha uchafu kutoka kwa jina la Pentekoste.

¹¹⁶ Huyo mwanamke alihofu, akawaza, “Loo, sasa nimefanya nini?” Labda, nasi tunamwona basi...Kama angalisogeza kidole kimoja cha mguu, angeliruka juu na kutoka humo, namna *hiyo*. Lakini Yeye hakufanya hivyo, alitulia tu kabisa na kumwangelia, alikuwa tu akiangalia yale aliyokuwa akifanya.

¹¹⁷ Sasa, wakati kimya kinapokuja, anashangaa, “Ni kitu gani kilichotukia sasa?” Naye anaangalia juu, “Atasema nini?” Ninamwona akiinuka, anasimama. Yuko sakafuni, nywele zake nzuri zimeshuka kote kuuzunguka uso wake, machozi yamekata kupitia kwenye milia ya uso wake, macho yake makubwa yalikuwa yakimtaazama Yeye, “Loo, Yeye atanitupa nje? Yeye atafanya nini kwa ajili ya huduma hii? Loo, nilitaka tu kufanya hivyo, kwa sababu ni—ninajua Yeye alimsamehe mwanamke kama mimi wakati mmoja. Nami ninajua Yeye ni Mungu, na—na laiti ningeweza kufanya jambo fulani! Na kwa sababu nimefanya hivyo, loo, ninahofia kitakachotukia.”

¹¹⁸ Anasimama, anaangalia kote, akasema, “Simoni, nina jambo la kukwambia.” Loo, haleluya! “Nina jambo la kukwambia. Ulinialika hapa kama Mgeni wako, nami nikaacha uamsho Wangu nije niwe Mgeni wako. Niliwaacha wale waliokuwa wakilia na kusihhi nikae, nije niwe Mgeni wako kwa sababu ulinialika Mimi. Niliwaacha wale waliokuwa na njaa na kiu, nije kwako. Nami nilifika hapa kwa wakati mzuri,” kama Yeye alivyo katika siku hizi za mwisho, “Nilikuwa hapa kwa wakati mzuri kabisa, lakini nilipofika, hakuna mtu aliyetawadha miguu Yangu, hawakutaka. Na halafu hapakuwapo na mtu aliyetia mafuta kichwa Changu, hapakuwapo na mtu wa ku—ku—kutia mafuta kichwa Changu, wala, wala shingo Yangu, na kuupangusa uso Wangu, nipate kukubalika kwa watu.

¹¹⁹ “Basi, Simoni, nilipoingia mlangoni, hukuwa umesimama pale kunikaribisha. Hukuwa umesimama pale, Simoni, ulivutiwa sana na huo mradhi mpya wa ujenzi na mambo fulani mnayoendeleza, ulivutiwa sana na kupata washiriki zaidi katika shirika lako. Hukuwa pale kunibusu Mimi. Ulinionea aibu mbele ya kundi hili, hukuwapo ku—kunikaribisha, kunibusu ningie moyoni mwako, kunikaribisha. Lakini tangu niliponinii. . . mwanamke huyu alipoingia,” (Yeye alijua alikuwa ni nani. Sasa, vipi kuhusu Nabii?) “ameendelea kuibusu miguu Yangu, hajakoma, bali ameibusu, akaibusu, akaibusu miguu Yangu. Hukunipa maji yoyote ya kuitawadha miguu Yangu, bali ameitawadha kwa machozi yake. Hukunipa *upako* wowote, bali ameendelea kunipaka mafuta tangu nimekuwa hapa. Nami najua yeye ni mwanamke mbaya, lakini nawaambia. . .” Loo, jinsi alivyokemea Simoni, jinsi alivyokataliwa!

¹²⁰ Sasa anamgeukia, nayo macho Yake yanamwangazia. Na, loo, hebu nisikie jambo hili, hebu hili na liwe—hebu hili na liwe ni lile atakaloniambia kwenye ile Siku: “Ninyi ndio mlinialika Mimi, ninyi wafuasi wa kanisa, mlinialika Mimi, bali hamkunikaribisha. Hamkuiosha miguu Yangu, hamkunipa kitu cha kujisafisha kwacho, hamkunipa nafasi ya kuzungumza kupitia kwenu, na mambo mengine ya kufanya. Msingefanya hivyo, maana mlinionea aibu. Mliniacha niketi pembeni na miguu michafu, lakini mwanamke huyu ameendelea kuiosha miguu Yangu kwa machozi ya macho yake, yale maji mazuri safi sana ya toba, akayapangusa kwa nywele za kichwa chake. Amin nawaambia, dhambi zake, ambazo zilikuwa nyingi, zimesamehewa zote.”

¹²¹ Hilo ndilo ninalotaka Yeye aniambie: “Dhambi zako, ambazo zilikuwa nyingi, umesamehewa zote.” Sitaki kuwa wa tabaka la juu, sitaki kuwa mfuasi wa *hili-na-hili*, kusudi wanasema, “Yeye alikuwa mfuasi wa *hili*,” Ninataka tu kuyachukua maisha yangu na kumwosha miguu Yake, yale niliyobakisha. Kwenye Siku hiyo, ninataka kumsikia akisema, “Dhambi zako, ambazo zilikuwa nyingi, zote zimesamehewa.”

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja tu.

¹²² Tuko kwenye kiamshakinywa hiki asubuhi ya leo, wageni walioalikwa, naye Yesu yupo hapa, kwa shukrani macho yamelowa, leso zinayapangusa macho. Ni kitu gani? Ni Yesu katika umbo la Roho Mtakatifu.

¹²³ Loo, Simoni, ama maskini mwanamke ama mwanamume ambaye kamwe hajamkubali, kwa nini usifanye hivyo sasa? Hii ni fursa yako. Tunapoomba, uko wapi? Anakuona, anaujua moyo wako. Wakati kila jicho limefumbwa, na vichwa vimeinamishwa, wakati huu mkuu, ni wangapi hapa ndani wasiomjua Yeye ambao wangetaka tu kusema, “Bwana Yesu, ningetaka kuiosha miguu Yako asubuhi ya leo kwa toba yangu.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Unataka kuinua mkono wako upesi sana, na kusema, “Niombe, Ndugu Branham?”

Mungu akubariki, Mungu akubariki. Mungu akubariki, akubariki. Wengine ungeinua mkono wako, useme. . . Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe.

¹²⁴ Wengine nyuma kwenye mkono wangu wa kulia, nyosha mkono wako, useme, “Jésus, Ee Jésus, Wewe ni Bwana wangu! Nimesimama mara nyingi wakati nilipokuonea aibu. Nimewasikia watu wakitumia Jina Lako bure, hata ni—niliona aibu kusema lolote kulihusu, nasikitika nilifanya hivyo, Jésus. Ninatubu, hivi hutanipokea?” Je, utainua mkono wako, useme, “Nikumbuke, Ndugu Branham,” unapoomba?

¹²⁵ Nyuma mkono wangu wa kulia, huko kwenye kusanyiko, ninaiona mikono yenu. Mungu awabariki. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, Dada. Mungu akubariki, Ndugu. Mungu akubariki, Dada. Mungu akubariki, mwingine. Mungu akubariki, Ndugu. Mungu akubariki, Ndugu. Kunaweza kuwa na wengine zaidi? Inueni tu mikono yenu, kisha muiweke chini.

Moja kwa moja mbele yangu sasa, Mungu akubariki. Mungu akubariki. “Jésus!” Mungu akubariki, naam, bwana. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

¹²⁶ Mkono wangu wa kushoto, Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Bwana akubariki, Dada. Mungu akubariki, huko nyuma kabisa. Mungu akubariki, naam, ninakuona, huko karibu nyuma ya kivuli hapo, bali Mungu anakuona. Mungu akubariki. Kote jengoni: “Jésus, asubuhi ya leo ninatubu.”

¹²⁷ Ni wangapi wenu ninyi washiriki wa kanisa sasa? Baada ya wenye dhambi thelathini au arobaini kuinua mikono yao, vipi kuhusu ninyi washiriki wa kanisa ambao mmekuwa na nafasi mbele ya wengine kulidai Jina la Yesu, lakini uliona aibu, na kugeuza kichwa chako, na kuondoka? Tunazungumza juu ya uponyaji wa Kiungu ama nguvu Zake, unaona tu aibu kidogo kusema, “Mimi ni Mpentekoste.” Unasema, “Jésus, nilikuacha uketi hapo pia, bali kamwe sitafanya hivyo tena. Nimetubu, jalia niioshe miguu Yako, Jésus.”

¹²⁸ Hebu mfuasi wa kanisa ainue mkono wake kwamba umeona aibu, na...Mungu akubariki. Mungu abariki... Hayo ni maungamo halisi. Mungu akubariki, hilo ni jema. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Naam, naam. Mungu akubariki. Mungu akubariki, kila mahali. Washiriki, naam, Mungu awabariki. "Nimeikwepa nafasi hiyo. Niliona aibu, ilikuwa ni bosu wangu, ama ilikuwa ni jirani yangu, na—nao wakasema mambo maovu kuhusu mkutano, lakini sikusema lolote, nilitulia tu na kuendelea. Lakini tangu sasa na kuendelea, sitafanya hivyo, nitalitetea Jina la Yesu, nitafanya hivyo. J sus, ninataka kuninii...Ninataka unichukue asubuhi ya leo, ninakutaka Wewe, uniambie nimesamehewa." Hilo ni zuri. Mungu awe pamoja nanyi.

Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, nami ninawatakeni mtubu moyoni mwako:

. . . doa moja jeusi,
Kwako Wewe, ambaye Damu Yako inaweza
kusafisha kila doa,
Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Naja!
Jinsi nilivyo mimi, Wewe uta. . .

Kamwe hatakukataa.

. . . pokea;
Utawakaribisha. . .

Dhambi zetu ambazo ni nyingi zote zimesamehewa.

. . . safisha, pokea;
Kwa sababu ninaahidi ninaamini,
Ee Mwana-Kondoo. . . Mungu, naja! Naja!

[Ndugu Branham anavumisha—Mh.]

¹²⁹ J sus, wengi hapa asubuhi ya leo wametambua ya kwamba wamekuacha Wewe ukiketi, walikupita, bali hawatafanya hivyo tena, Bwana, kamwe, watakumbuka maskini mkahawa huu katika chumba hiki cha shule, alichopitia J sus. Waliahidi wataamini, walitaka kukumbukwa katika maombi. Waliinua mikono yao kwa Mungu, wakisema ya kwamba "Sasa na—na—naamini, najisalimisha, Bwana. Nime—nimemalizana na maisha ya kutokuamini, naja kama mtumishi Wako sasa."

¹³⁰ Watu wengi, hata nimewaona wahudumu wakiinua mikono yao, kwamba waliona aibu kwa nafasi walizokuwa nazo kushuhudia, mambo ambayo wamefanya, washiriki wa kanisa, lakini hata hivyo ni wazembe. Tusamehe sisi sote dhambi hiyo, Bwana. Tusamehe hiyo, ili tuweze kutoka hapa tukiwa mtu bora zaidi, tukijua ya kwamba. . .

¹³¹ Tulikualika hapa chini asubuhi ya leo, tulikualika, uje, Chicago kwenye mkutano huu pamoja nasi. Usiku baada ya usiku, siku baada ya siku, tunaona mkono Wako mkuu ukitenda kazi miongoni mwetu, tunajua ni Wewe. Nasi tunashukuru sana,

Bwana, tu—tunakukaribisha tu, tunakushukuru tu kwa mioyo yetu yote.

¹³² Tunaomba sasa ya kwamba utawabariki watu hawa. Jalia wachukue kanisa zuri la nyumbani mahali fulani, kanisa zuri la Full Gospel, wawe watumishi Wako na kuishi kwa ajili Yako mpaka Siku ile tutakapokutana tena. Huenda tusikutane kwenye kiamshakinywa kingine, lakini tuta—tutakutana Usiku fulani kwenye Karamu, Karamu ya Arusi.

¹³³ Ninaomba, Mungu, mpaka wakati huo, kwamba neema ya Mungu itatupa nguvu na ushuhuda wa kutosha kumsifu Mungu wetu, na kuishi kwa ajili Yake wala kamwe tusimwonee aibu, kwa kuwa ninawakabidhi watu hawa Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, mimi mwenyewe pamoja nao, Bwana. Ninajitoa mwenyewe kama utumishi, mimi hapa, Bwana, baada ya kuwaombea, chukua maisha yetu pamoja, jalia yatumiwe kama kitambaa cha kupangusia, Bwana, kwa miguu Yako, kitambaa tu cha miguuni, chochote kile, Bwana, chochote kile. Haidhuru watu wanasema nini juu yetu, jalia tuishi, na tumwishie Yesu, ambaye ameiosha mioyo yetu asubuhi ya leo kwa msamaha wa dhambi zetu. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alipenda kwanza . . . (Unamaanisha kwa moyo wako wote?)
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Hebu tuinue mikono yetu sasa na tuuimbe.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹³⁴ Sasa, hebu tu, katika utamu wa ushirika, tugeuke moja kwa moja, wakati tukiwa, tuuimbe tena, na kupeana mikono na mtu fulani karibu nawe, ukisema, “Salamu, raia mwenzangu wa Ufalme.”


¹³⁵ Hao watu mlioinua mikono yenu, hakikisheni kwamba mnapeana mkono na mtu mwingine, useme, “Nilikuwa mmoja niliyeinua mkono wangu. Je, naweza kwenda kanisani kwenu?” Au wewe uwaalike kama wakikwambia hivyo, lifanye.

¹³⁶ Tafuta mhudumu mzuri ambaye atakubatiza katika ushirika wa waaminio, na hapo Mungu atakubatiza kwa Roho Mtakatifu. Hebu na tumwishie siku zetu zote, haidhuru gharama yake ni nini, hatujali, tunatahayarika, ama chochote kulihusu, ishi tu maisha hayo mazuri na umwishie Yesu.

Nampenda, (Mungu akubariki, Joseph.)
Nampenda
Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Wote wanaoamaanisha hilo kweli, inua mkono wako sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari. 

61-0429B Mmoja Wa Watu Katili Sana Mjini
Stephen Mather High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org